AMANI KATIKA JAMII

Na
Abdulla Talib Abdulla

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyetuumba mataifa na makabila mbali mbali ili tujuwane na kushirikiana. Sala na Salaam zimshukie Mtukufu wa daraja, Mtume wetu na kigezo chetu, nabii Muhammad S.A.W. pamoja na wafuasi wake wote hadi kitakaposimama kiama. Ama baada ya hayo.

Mwanadamu ni mwanajamii katika maumbile yake, anazaliwa katika jamii, anaishi na hufia humo. Kwa msingi huo jamii ni lazima itunzwe, ienziwe na ihifadhiwe ili idumu katika uasili wake. Uasili ambao ameutaja Allah SW pale aliposema***: ((Kwa hakika tumekuumbeni kutokana na mwanamme mmoja na mwanamke mmoja na tukakujaalieni mataifa na makabila mbali mbali ili mjuane, hakika mbora wenu mbele ya Allah ni yule mchaji zaidi)){Al-Hujuraat:13}.***

Ni jambo lisilo na shaka kuwa jamii yetu imeundwa kwa watu wenye itikadi, imani na mitazamo tofauti katika nyanja zote zikiwemo za dini, fikra,mila n.k. Vitu hivi vimo ndani ya nyoyo zetu, na vinatembea katika damu zetu. Tofauti hizi zinapaswa kuheshimiwa na kuvumiliwa na walio upande mwengine, ilimradi hazikiuki sharia zilizopo, kwani ni katika jumla ya uhuru aliotupa Allah SW aliposema: ***((Hakuna kulazimishana katika kufuata dini)) {Baqara: 256}.*** Illivyokuwa dini hailaimishwi nalo ndilo jambo muhimu kabisa, hivyo mambo mengine yakiwemo kufuata rai, itikadi au mitizamo Fulani niawla zaidi kutokulazimishwa Hivyo, sote tutabaki kuwa ni watu wa jamii moja ambayo yapo mengi yanayotuunganisha na hatupingani nayo; kwa vile yanapokuwepo hutuletea faida sote na yakikosekana hutokea hasara na ufisadi kwa wote. Lakini pia tukubali yapo tunayotofautiana na pengine tofauti zetu ni kichocheo kikubwa cha maendeleo iwapo tofauti hizo hazitogeuzwa uhasama.

Mwenyezi Mungu amemkirimu mwanadamu kuliko viumbe vyake vingi kama alivyosema: ***((Bila shaka tumemkirimu mwanadamu)) {Israa: 70}.*** Katika kumkirimu huko, amempa akili na utambuzi na akamteremshia Mitume na vitabu ili viwaongoze watu katika haki. Hivyo sharia, kanuni na taratibu ni lazima ziwepo, zifuatwe na zisimamiwe ipasavyo ili zilete haki ambayo hudumisha amani na ustawi mzuri wa jamii. Kukosekana kwa hayo kutapelekea nafsi kufuata matamanio na matokea yake ni kama alivyosema Mwenyezi Mungu ***((Na lau kama haki (Sharia) ingefuata matamanio yao basi vingeharibika (vilivyomo) mbinguni na ardhini)) {Al-Muuminuni: 71}.***

Amani ni kitu cha awali kinachotafutwa na mtu na jamii yoyote. Amani ndio chachu ya maendeleo, kupatikana haki na kuleta utulivu katika nafsi na jamii nzima. Kwa msingi huo nabii Ibrahim A.S alipowaweka watu wake katika jangwa

lisilo mti wowote aliomba kwa kusema ((***Mola wangu ujaalie mji huu kuwa ni wa amani na uwaruzuku watu wake katika matunda....)).*** Alitambua fika kuwa cha awali kinachohitajika ni amani kwani amani ndio itakayokupa nafasi ya kutumia kwa furaha rizki tofauti utakazoruzukiwa.

Kwa kiasi kikubwa jamii yetu inaishi katika amani, ingawa yapo baadhi ya mambo ambayo huihatarisha amani hiyo. Tusipokuwa makini na tukaipa nafasi migogoro na fujo kushika hatamu, jamii yetu itadumaa na kudharauliwa mbele ya jamii nyengine. Tutambue kuwa matukio yanayohatarisha amani yanapoachiwa, mwisho wake huwa ni mgumu na mchungu sana. Hivyo ni lazima tuyaepuke mambo yote ambayo ni vyanzo vya migogoro. Mambo hayo ni kama yafuatayo:-

1. Aswabia (Partisanship) – Na haya ni mahusiano/mafungamano yanayoletwa na ukabila, maumbile, rangi, ujimbo, tabaka n.k. Jambo hili lina ngvu za ajabu katika kuwaathiri na kuwakusanya watu (mobilization).
2. Habari na taarifa – Ni mtu au kikundi kupata taarifa zisizo na ukweli, kutokuwa na taarifa, kutokufahamu, kupotosha n.k.
3. Matakwa (interest) – Pale mtu au kikundi kinapoamini kuwa ili kitosheleze mahitaji yake ni lazima wengine/wenzake wajitolee (wakose) aidha chote au baadhi ya haki zao.
4. Miundo/Maumbo (Structural/Institutional) – Husababishwa na mijengeko ya jamii, taasisi n.k. Aidha kanuni, tafsiri, mazingira halisi, mabadiliko n.k. Aina hii imechukuwa nafasi kubwa katika ulimwengu wa sasa.

Kwa kujua madhara ya migogoro tutaona kuwa dini imeziba kila njia inayopelekea kwenye mgogoro na hatimae fujo. Hivyo imesisitiza zaidi kuzuwia kabla haujatokea na uliopo usimamishwe ili usikuwe. Aidha ukiishatokea imesisitiza kuleta suluhu kwa mazungumzo, kutumia sharia na pengine nguvu kama kutumia adhabu, vikwazo n.k ilimradi usiendelea au kukua zaidi.

Tunapouangalia Uislamu tutakuta kuwa umezuwia vyanzo vya migogoro kwa mfano:-

- Aswabia: Kwa kujenga mafungamano na mashirikano ya kijamii chini ya misingi inayowaunganisha wote.
- Habari: kufanya utafiti wa kina juu ya habari yoyote, uwazi na kujifunza.
- Matakwa: Haki na uadilifu, kujenga jamii inayopendana n.k
- Muundo: Kwa kuweka nidhamu madhubuti inayofanya kazi kwa mujibu na maumbile ya mwanadamu na inayokubaliana na mabadiliko.

Mashirikiano ni nguzo muhimu sana katika kujenga jamii yenye nguvu na maendeleo. Mashirikiano hayo yanawahusu wanajamii wote kwa kuzingatia mipaka iliyowekwa na dini, kanuni na sharia nyenginezo zilizopo.

Tunapojiangalia hapa Zanzibar, pamoja na kuwepo waumini wa dini, itikadi, vyama vya siasa na fikra mbali mbali lakini tutagundua kuwa mambo yanayotuweka pamoja ni mengi zaidi. Sote tunahitajiana kwa njia mbali mbali katika maisha yetu ya kila siku. Zaidi ya hivyo, maadui wetu wa pamoja tukiwa waumuni ni wengi mno wakiwemo mahasidi, maradhi, ujinga na umasikini. Juhudi na mashirikiano tu ndio yatakayotuwezesha kuunganisha nguvu na kukabiliana nao.

Kuporomoka kwa Ukomunisti na kuenea kwa utandawazi kumepelekea wanadamu wawe wahanga wa matukio mengi bila ya kuangaliwa imani na itikadi zao. Uadilifu wa wanasiasa wa mataifa makubwa umekosekana na kinachojulikana sasa ni nguvu za biashara na kijeshi tu katika kujenga mamlaka za matakwa. Matokeo yake, tunakabiliana na zimwi ambalo haliangalii nyoyo za watu bali nyama na damu zao tu!

Hivyo waumini hasa tuliopo Zanzibar, ni vyema tuangalie yale ambayo yanatumaliza ili tukabiliane nayo badala ya kupoteza muda tukamalizana wenyewe kwa wenyewe tu. Tusiwe wepesi kusikiliza na kufuata kibubusa kwani Mtume SAW amesema: "*Asiwe mmoja wenu mwigo tu akisema mimi ni pamoja na watu wakifanya wema nami nitafanya wema na wakikosea nami nitakosea".* Uislamu haukubaliana na msemo wa 'kifo cha wengi harusi" bali kila mtu kubeba dhamana kwa analolifanya.

Ili kuelewa vyema maelezo haya, na tupitie mifano ifuatayo:-

- Sasa hivi kuna nchi ambazo zinavunja minara ya misikiti, jee itaishia nchini mwao au itaendelea na kwengine? Jee itaishia na minara tu au itakuja mpaka katika misikiti.
- Waumini hawapendelei zinaa, kubaribika maadili ya wanafamilia, mapicha machafu yanayosabazwa na magazeti au vyombo vyengine vya mawasiliano, utumiaji wa madawa ya kulevya n.k.
- Waumini wa dini zote hawapendelei kugubikwa na umaskini.
- Waumini wote hawapendi wakose ajira.
- Waumini wa dini zote wanaathirika na suala ya UKIMWI.
- Dini zote zinapinga suala la rushwa, kudhulumiana, mauaji ya watu wasio na makosa.
- Je ukosefu wa maji safi na salama, madawa hospitalini, elimu bora, makazi mazuri, mazingira safi yanaangalia imani au itikadi ya mtu? Jawabu ni kuwa, sote tunaathirika bila ya kuangalia imani ya mtu.

Hivyo basi, niruhusuni nihitimishe kwa kusema kuwa:
Yanayopaswa kutuunganisha ni mengi kuliko ya kutogombanisha. Kwa hivyo, mashirikiano kati ya Waumini wenye misimamo, itikadi na mawazo tofauti katika harakati za kijamii ni suala la muhimu na ni lazima. Ulazima unakuja pale tunapozingatia ukweli kuwa hakuna mja mwenye kila kitu. Hivyo tunahitajia

kuunganisha nguvu pale tunapokubaliana huku tukiheshimiana kwa iman na itikadii zetu.

Haki za binadamu zinajulikana kama ni stahili alizonazo binadamu kutokana na utu wake. Ni haki alizozaliwa nazo, kwa maana hiyo haki hizo zipo bila ya kujali kama sheria inazitambua au la.

Kwa mtizamo wa Kimagharibi, harakati za kupigania haki hizi zimeanzia siku nyingi hasa katika karne ya kumi na saba. Zilianza kwa kupigania Demokrasi na haki za kisiasa ili kuondoa tawala za kifalme na kidini huko Ulaya na kuweka taratibu za kuchagua kama mabunge na mabaraza ya wawakilishi. Baada ya vita vikuu vya pili harakati hizi zilipamba moto na kufikia makubaliano ya pamoja ya kulinda haki za binadamu kutokana na ukatili uliofanywa na madikteta mbali mbali. Tamko la kimataifa la haki za binadamu lilipitishwa mwaka 1948 na yakafuata matamko mengine na mikataba mbali mbali.

Tukiangalia misingi ya haki za binadamu katika Uislamu tutakuta kuwa Uislamu unafunza kuwa binadamu wote wana haki zao ambazo ni lazima zilindwe kama walivyokuwa na wajibu ambao ni lazima wautekeleze. Kwa mfano haki ya mtoto ya kupatiwa malezi na matunzo mazuri ni wajibu wa mzazi au Dola; haki ya raia kufanyiwa uadilifu na kupatiwa fursa sawa ni wajibu kwa kiongozi n.k.

Uislamu umebainisha haki hizi kwa amani na bila ya kuombwa na watu au harakati zozote kuzidai. Hivyo, haki za binadamu katika Uislamu ni katika mambo ya maumbile. Uislamu umejengea haki za binadamu katika misingi miwili mikuu nayo ni:-

- Itikadi ya tauhidi ambayo imelenga kumkomboa mwanadamu kutokana na utumwa wakumuabudia mwanadamu mwenziwe.
- Kutukuzwa na kukirimiwa binadamu kwa ubinadamu wake.

Kimsingi, Uislamu umempa haki binadamu hata kabla wazazi wake hawajaoana. Umewataka wachaguane kwa misingi ya tabia njema na imani kwa maslahi ya vizazi watakavyovipata. Haki za mtoto zikaendelea kulindwa tokea tumboni mwa mama yake, anapozaliwa, anapolelewa hadi anapokufa.

Hata binadamu anapokufa, bado Uislamu unamdhaminia haki zake ambazo ni lazima atekelezewe ikiwemo kukoshwa, kukafiniwa, kusaliwa, kuzikwa, kutekelezwa wasia wake, kulipiwa madeni yake na kugawiwa mali aliyoiacha kwa jamaa zake wa karibu. Aidha imeharamishwa kuvunjwa viungo vyake na kufanyiwa jambo lolote ambalo asingeliridhia kufanyiwa wakati akiwa hai.

Uislamu unamthamini binadamu kwa ubinadamu wake sio kwa mali yake, jimbo analotoka rangi au kabila lake n.k. Watu wote ni sawa katika ubinadamu wao hata wakati mwengine tofauti za dini hazitizamwi katika kutukuzwa kwa

ubinadamu. Mfano mzuri ni ***mafunzo ya Mtume S.A.W ambae siku moja lilipita jeneza mbele yake nae akasimama. Waliokuwa nae wakamwambia ni jeneza la myahudi; nae S.A.W akawauliza, jee yeye si binadamu? {Bukhari}.***

Uislamu umeamrisha kuhifadhiwa haki zote za binadamu ikiwa ni za kimali, kihali (nafsi), kidini, kidunia, kiakili au kimwili. Pia umetilia mkazo kuhifadhiwa mambo matano muhimu kwa binadamu ambayo ni dini, nafsi (kizazi), akili, mali na utukufu (heshima).

Baadhi ya haki za ujumla za kibinadamu ambazo zimetajwa na kusisitizwa katika Uislamu ni kama zifuatazo:-

- Haki ya kuishi/kuwa hai. (Nisaa: 29).
- Haki ya kufurahia maisha (Aaraf: 32 na Qaswas: 77).
- Haki ya uhuru wa kuamini (Insaan: 2 – 3 na Baqara: 256).
- Haki ya kupata elimu na kuitumia. Amesema Mtume S.A.W: ***Kutafuta elimu ni wajibu wa kila muislamu.***
- Haki yakuwa na maoni tofauti (Maida: 48).
- Haki ya ushauri na nasaha (Ala Imran: 159).
- Haki ya usawa kwa watu wote (Hujurat: 13).
- Haki ya uadilifu (Nisaa: 58 na Nahli: 90).

Hizi ndizo baadhi ya haki za ujumla katika mtazamo wa haki za binaadamu ndani ya Uislamu. Bila ya mtu kuzipata haki hizi hapatokuwa na mategemeo ya mafanikio katika jamii na kwa hivyo utumiaji wa nguvu ndio utakaotumika ambapo matokeo yake ni kuvunjika kwa amani na kuzagaa fujo na hatima yake ni jamii kukosa maendeleo.

Tunamuomba Mola wetu atuthibitishe katika haki na kuifuata, atashushie amani na utulivu katika nchi yetu na atujaalie kutajwa kwa wema na watakaokuja baada yetu. Amin.